**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA Ibada Ya Kumshukuru Mungu Kwa Ajili Ya Askofu Method Kilaini, Askofu Msaidizi Wa Jimbo Katoliki La Bukoba, Kufikisha Miaka 50 Ya Upadre

**BUKOBA, KAGERA**
**TAREHE 19 MACHI 2022**

**Mhashamu Baba Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya na Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC);**

**Wahashamu Maaskofu Wote;**

**Mhashamu Baba Askofu Method Kilaini, Askofu Msaidizi wa Jimbo la Bukoba na Maaskofu Wasaidizi wote mliopo;**

**Waheshimiwa wawakilishi wa majimbo, Mamonsinyori na watawa wote;**

**Waheshimiwa viongozi wetu wa dini wote wa madaraja mbalimbali mliohudhuria hapa;**

**Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;**

**Waheshimiwa Wabunge;**

**Mheshimiwa Meja Jenerali Charles Mbuge, Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Kagera;**

**Prof. Faustine Kamuzora, Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera na Viongozi wote wa Serikali mliopo;**

**Viongozi wa Halmashauri za Walei na waumini wenzangu;**

**Wageni waalikwa, mabibi na mabwana.**

**TUMSIFU YESU KRISTU!**

***Ba-tata Mwasibamuta! Ba-mae Masibota! Mshanage! (mchana)***

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, neema na afya njema na pia kutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo kushiriki pamoja na mtumishi wake Mhashamu Baba Askofu Method Kilaini, Askofu Msaidizi wa Jimbo Katoliki la Bukoba, katika ibada ya misa takatifu ya kumshukuru Mungu kwa kutimiza miaka 50 ya upadre.

Naomba nitumie fursa hii kuwaletea salamu kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye anakupongeza sana Baba Askofu Kilaini kwa kutimiza miaka 50 ya upadre. Anakutakia afya njema unapoendelea kulitumikia Kanisa Katoliki na Watanzania. Mheshimiwa Rais, alipenda sana kuhudhuria maadhimisho haya, lakini kutokana na majukumu mengi ya kitaifa aliyonayo amenipa mimi heshima ya kumwakilisha

na ninakushukuru Baba Askofu Method Kilaini kwa kuridhia. Ninajisikia furaha sana kutumwa kushiriki tukio hili muhimu.

***Wahashamu Baba Maaskofu Wakuu, Maaskofu, viongozi wote, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

Nilipotumwa na Mheshimiwa Rais nije hapa nilijiuliza: Sasa kwa huyu Baba, Mtaalamu aliyebobea, mwenye shahada ya Udaktari wa Tauhidi katika Historia ya Kanisa, tena kutoka chuo kikuu maarufu cha Gregoriana kule Roma na Kasisi kwa kipindi cha nusu karne, nitaenda kumwambia nini asichokijua? Mwanzo niliwaza labda nije tu niseme *Tumsifu Yesu Kristu na kutoa pongezi halafu niombe kuketi!* Lakini kama ningefanya hivyo, aliyenituma nije kumwakilisha asingenielewa na ninyi pia msingenielewa. Hivyo, sina budi kusema kidogo.

**Jambo la kwanza**, naungana na Mheshimiwa Rais, pamoja na Kanisa zima kumshukuru Mungu na kukupongeza Baba Askofu Method Kilaini kwa kutimiza miaka 50 tangu ulipopata daraja takatifu la upadre tarehe 18 Machi, 1972 ukiwa kijana wa miaka 24 tu! Hongera sana *Waitu ta-Askofu Kilaini, mayo muno!* Hapa, tunapata fundisho kubwa hasa kwa vijana na hata sisi watu wazima tuliozaliwa kabla ya zama hizi za Kompyuta (BBC). Huyu kijana wa zamani, kule Dar es Salaam tulikuwa tunamuita MK Chimbachimba na sasa Mhashamu Askofu Msaidizi wa Jimbo hili, alisikia wito wa Mungu na akajitoa kulitumikia Kanisa. Mwenzetu alielewa mapema neno la Mungu tunalosoma katika Biblia Takatifu Kitabu cha Mhubiri (Au Kohelethi) sura 11:9-10 na sura 12:1, naomba kunukuu: *"Wewe kijana, uufurahie ujana wako, na moyo wako ukuchangamshe siku za ujana wako, ukaziendee njia za moyo wako na katika maono ya macho yako. Lakini ujue wewe ya kwamba kwa ajili ya hayo yote, Mungu atakuleta hukumuni. Kwa hiyo ondoa majonzi moyoni mwako, nawe uondoe ubaya mwilini mwako, kwa maana ujana ni ubatili, na utu uzima pia. 12:1 Mkumbuke muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja siku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakayosema "Mimi sina furaha katika hiyo".* Hivyo, katika fahari yenu ya macho ninyi vijana wa kizazi kipya najua mnaona na mnatamani vingi (*Abaisiki balungi, abasigazi ebikaka*, mali na maisha mazuri kama *Abalangila*). Nafahamu pia wengi wenu vijana mnatumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii. Vijana Wakatoliki wa Jimbo la Bukoba: Mpo? *Mapendo … Daima*. Hivyo kwa mfano wa kijana Method wa enzi hizo, yatupasa nasi tukumbuke hayo tuliyoaswa na Mhubiri!

**Jambo la Pili**: Napenda nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali kukushukuru kwa dhati Baba Askofu Kilaini kwa mchango wako maridhawa katika Kanisa na pia kwa jamii ya Watanzania. Serikali inakushuru kwa kuwa miongoni mwa

waanzilishi wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini (1994) ambayo imeimarisha maelewano miongoni mwa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali hapa nchini. Aidha, Serikali inakushuruku pia kwa kuwa miongoni mwa waanzilishi wa Tume ya Kikristo ya Huduma za Jamii - *Christian Social Service Commission* (1992) ambayo imefanya kazi kubwa katika kuongeza ufanisi na ubora wa utoaji huduma kwa jamii.

**Jambo la tatu:** Katika kipindi cha miaka 50 ya utumishi wako, umefanyika baraka kwa Kanisa na Taifa letu kupitia utume wako. Utume wako umeacha alama chanya katika maisha ya wengi uliowahudumia sehemu mbalimbali. Umekuwa mwalimu hodari kwa sisi waumini. Kupitia uandishi wako mahiri, na mafundisho yako fasaha kupitia Redio na Televisheni mbalimbali za Kanisa umetuongezea uelewa wa imani yetu. Aidha, tunashukuru pia kwa vitabu vyako ambavyo vimeendelea kutumika katika mashule yetu kutoa elimu ya jamii kwa ajili ya kujenga maadili mema kwa vijana wetu. Vilevile, tunakushukuru kwa jitihada zako za kuimarisha Jumuiya ndogo ndogo za Kikristo. Sina shaka kuwa kwa neema ya Mungu utaendelea kutumika na kugusa maisha ya wengi Zaidi mpaka uifikie ile tuzo kama tunavyosoma katika waraka wa mtume Paulo kwa Wafilipi 3:13-14 *"Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele; nakaza mwendo, niifikie tuzo la thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu"*. Ta-Askofu Method, sina mashaka kwamba utaendelea kutumikia wito wako ukiongozwa na Roho wa kweli.

***Wahashamu Maaskofu na Mapadre wa Jimbo la Bukoba;***

Naomba pia niwapatie changamoto moja wana Jimbo hili la Bukoba ambalo lina historia kubwa sana. Nafahamu Mhashamu Baba Askofu Kilaini umeandika vitabu vinavyoelezea historia ya Jimbo hili na nafasi yake katika kueneza injili. Tunakupongeza sana na tunakushukuru! Lakini sasa naliomba jimbo hili lifikirie kuwa na Makumbusho makubwa yatakayolingana na ukubwa wa historia hiyo! Naamini kwa kupitia Makumbusho hayo, waumini, wanazuoni na wananchi kwa ujumla watapata fursa ya kipekee kuijua historia ya Kanisa, mkoa huu wa Kagera na mchango wake katika Taifa la Tanzania kwa undani zaidi.

***Wahashamu Baba Maaskofu Wakuu, Maaskofu, viongozi wote, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

**Jambo la nne:** Kwa niaba ya Serikali napenda kuwapongeza na kulishukuru Kanisa Katoliki kwa kuunga mkono juhudi za Serikali na kwa kutoa mchango mkubwa sana katika ustawi wa Taifa letu kiroho, kiuchumi na kijamii. Kanisa limeweza kufikisha huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali nchini,

yakiwemo yale ambayo Serikali bado haijaweza kufikisha huduma hususan vijijini na maeneo wanakoishi watu wa hali ya chini mijini. Wananchi wameweza kupata huduma nzuri za afya na elimu hasa kwa watu wa kawaida, yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Mwenyezi Mungu azipokee kazi zenu njema. Naamini wengi wetu hapa tumefaidika na huduma hizi za Kanisa. Mimi binafsi ni tunda la Kanisa. nilisoma elimu ya Sekondari hadi Kidato cha 4 katika Seminari ya Mt. Yosefu Ujiji na ile ya Mt. Karoli Lwanga Itaga Tabora. Hata Kidato cha 5 na 6 nilipata elimu hiyo katika Shule ya Sekondari ya Ihungo hapa Bukoba (zamani ilimilikiwa na Kanisa Katoliki ikijulikana kama St. Thomas More College) na baadhi ya walimu wangu wakiwa Mapadre (Fr. Peter Rutayongororwa na mwingine Fr. Ignas).

***Wahashamu Baba Maaskofu Wakuu, Maaskofu, viongozi wote, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

**Jambo la tano:** Nafahamu katika jimbo Katoliki la Bukoba na katika majimbo mengine, Kanisa linajishughulisha na mambo mbalimbali ya kimaendeleo ikiwemo miradi ya vikundi vya vijana na akina mama, kilimo bora na ufugaji wa kisasa. Pamoja na kwamba shughuli hizi zimewasaidia watu wengi kutoka katika lindi la umasikini, Serikali inaona kuwa, uchumi na maisha ya wana Jimbo na mkoa wa Kagera kwa ujumla yanaweza kuboreshwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Mkoa huu wa Kagera unapakana na nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Bila shaka hii ni fursa kwa Mkoa wetu kuwa kitovu cha biashara. Jana nilikwenda Mutukula kuzindua jengo zuri la Kitegauchumi lililojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa. Aidha, nilipita kujionea fursa za utalii kwenye maporomoko ya maji Kyamunene na shughuli za uhifadhi wa mazingira na kilimo cha miti. Ninafahamu pia wananchi wa Mkoa wa Kagera ni wafanyabiashara na wajasiriamali wazuri. Hata wana Kagera walioko nje ya mkoa na hata nje ya nchi tunawaona wako vizuri (*abalangila*)! Na hakika wanaweza kufanya zaidi kuinua Kagera. Kwa upande wa Serikali, tumejielekeza katika kuboresha na kujenga miundombinu ya usafiri na usafirishaji, miundombinu ya Elimu, afya na maji, ili kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na uchimbaji wa madini kama mgodi wa Nikel Kabanga na kufungua fursa za biashara na ajira. Katika hili la uwekezaji mkubwa Serikali inatilia mkazo ushirikishwaji na uwezeshaji wa wananchi (local content) ili waweze kweli kunufaika na uwekezaji huo. Aidha, kuhusu usafiri na usafirishaji, jana nilipokuwa nikizungumza na Wananchi katika viwanja vya Mayunga hapa Bukoba, niliwatangazia Wananchi kuhusu uamuzi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan kuelekeza kwamba ujenzi wa mradi wa stendi ya mabasi ya Bukoba uliokuwa umekwama kwa muda mrefu uanze kutekelezwa na analeta jumla ya Shs. Bilioni

moja kwa mwaka 2022/23. Serikali pia inakamilisha mazungumzo na Benki ya Dunia kupata fedha za kuboresha huduma muhimu katika miji yetu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa soko la kisasa hapa Bukoba.

***Wahashamu Baba Maaskofu Wakuu, Maaskofu, viongozi wote, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu naomba kutumia nafasi hii kuwakumbusha mambo matatu, nikiwaomba myatilie msisitizo zaidi katika mafundisho na maonyo yenu kwa waumini na watanzania kwa ujumla.

**Kwanza,** ni umuhimu wa kipekee wa kulinda na kudumisha amani katika nchi yetu. Amani ni suala muhimu sana. Bila ya amani hakuna maendeleo. Bila amani, hata haki na uhuru wa kumwabudu na kumtukuza Mungu wetu utakuwa mashakani. Hivyo, hatuna budi kusimamia haki sambamba na kuenzi na kuitunza amani yetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo. Kwa sababu hiyo, nawasihi sana ninyi viongozi wetu wa dini kutukumbusha mara kwa mara sisi waumini, na watu wote, kuhusu umuhimu wa kusimamia haki na kudumisha amani aliyotuachia Bwana wetu Yesu Kristu na pia kuiombea nchi yetu na viongozi wake, kupitia kwa Mama Bikira Maria msimamizi wa Taifa letu.

**Pili,** ninawaomba msichoke kufundisha na kulea vijana katika maadili mema na kuthamini kufanya kazi halali. Katika nyakati hizi, ni ukweli ulio wazi kuwa kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii yetu. Vitendo viovu na mambo yasiyompendeza Mwenyezi Mungu yanazidi kuongezeka. Mambo ambayo siku za nyuma yalikuwa nadra sana kutokea au kusikika sasa yanakuwa habari za kila siku na wakati mwingine huonekana ati ni kawaida. Watoto kutokuheshimu wakubwa, wazee kutokujiheshimu, ulevi, vitendo vya rushwa, uvivu, wizi na ufisadi, mauaji ya kutisha na idadi kubwa ya ndoa kuvunjika na kuongezeka kwa watoto wa mitaani ni vielelezo dhahiri vya kuporomoka kwa maadili katika jamii yetu. Kushuka kwa maadili ni jambo lenye athari mbaya kwa jamii na Taifa kwa ujumla, hivyo kunachangia sana na kurudisha nyuma juhudi za kujiletea maendeleo nchini mwetu. Kunaifanya kazi ya kuondoa umaskini kuwa ngumu mithili ya msalaba wa zege!

Mimi naamini kwa dhati kuwa watu, ikiwa pamoja na sisi viongozi wa Serikali na wa vyama vya siasa wakishika mafundisho ya dini, wakawa na hofu ya Mungu, maovu mengi yatapungua sana na nchi yetu itaongozwa vizuri. Ndiyo maana naendelea kuwaomba kwa niaba ya Serikali, viongozi wa dini zetu zote tusaidiane kulea Taifa letu kimaadili. Tuweke mkazo zaidi kwa vijana kwa sababu, kwanza wao ndio wahanga wakuu wa maovu yanayotendeka. Lakini pili,

wao ndio Taifa la leo na viongozi wa kesho. Tukiwaandaa vyema, mustakabali wa Taifa letu na watu wake utakuwa kwenye mikono salama. Tukishindwa leo, tutalia na kusaga meno kesho. Uhai wa Taifa letu utakuwa mashakani.

**Tatu,** Ni kuhusu usafi na utunzaji wa mazingira. Tunaomba Viongozi wa Kanisa Katoliki na madhehebu mengine yote ya dini mpaze sauti kuhamasisha usafi, ulinzi na uhifadhi wa mazingira katika nchi yetu. Katika dini zote, Mwenyezi Mungu alitupatia dunia nzuri na akatuamuru tuitunze. Ndivyo tunavyosoma katika kitabu cha mwanzo 2:15 *"Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamuweka katika bustani ya Edeni ailinde na kuitunza*". Hivyo, nawaomba ninyi mlio mawakala wa Mwenyezi Mungu hapa duniani muwaongoze waumini na kuwahimiza kuitunza ekolojia ya nchi yetu nzuri kwa kutunza misitu, na vyanzo vya maji, kupanda miti; na kufanya usafi wa mazingira yetu wakati wote.

***Wahashamu Baba Maaskofu Wakuu, Maaskofu, viongozi wote, wageni waalikwa, mabibi na mabwana;***

Naomba sasa nimalize hotuba yangu kwa kuwakumbusha waumini wenzangu kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Mapadre na Viongozi wote wa Kanisa, kuwatia moyo na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili waendelee kuifanya kazi ya Bwana kwa uhodari na kuliletea Jimbo letu la Bukoba na Taifa kwa ujumla maendeleo endelevu ya kiroho na kimwili.

Kwa niaba ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba yangu binafsi, nakuombea Baba Askofu Mjubilei wetu afya njema na utume mtakatifu katika siku zako zote hapa duniani. Kwa mara nyingine tena, hongera sana kwa Jubilei yako ya dhahabu ya Upadre. *Waitu ta-Askofu Method Kilaini mayo muno.*

Mwisho kabisa kwa heshima na kwa kutambua kuwa bado una nguvu za kulima katika shamba la Bwana na kumrudishia Mungu mavuno mengi zaidi, naomba upokee zawadi ndogo kwa utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristu. Ukiridhia naomba niifungue!

**TUMSIFU YETU KRISTU**

**Asanteni sana.** ***Nimbasima muno mwakola.***